# "ULEMAVU BARANI AFRIKA"

# EPISODE 3: " Kale walinikubali, sasa wananitenga "

**AUTHOR: Chrispin Mwakideu**

**EDITORS: Andrea Schmidt, Aboubakary Liongo**

**List of characters / Episode 3:**

**MSIMULIZI**

**<u>SCENE ONE : SUNDAY MORNING AT KAREMI'S HOUSE</u>**

- Zabibu (MKE, 15)
- Theresa (mke, 60)
- Karemi (mume, 18)

**<u>SCENE TWO : AT THE HOSPITAL ENTRANCE</u>**

- Oluanda (mume, 18)
- Tofa (mke, 40)
- Karemi (mume, 18)

**<u>SCENE THREE : AT CHITOTO'S HOMESTEAD</u>**

- Fagilio (mume, 42)
- Chitoto (mume,19)

**<u>SCENE FOUR : OUTSIDE OLUANDA'S / KAREMI'S HOME</u>**

- Magoto (mume, 18)
- Oluanda (mume,18)
- Tofa (mke, 40)
- Karemi (mume,18)
- Kangwa (mke,18)

**UTANGULIZI:**

Salamu kemkem na shukrani kujiunga nasi katika kipindi cha **Noa bongo, jenga maisha yako**. Tunaendelea na mchezo wetu kwa jina " **Ulemavu barani Afrika** " Kipindi kilichopita, Oluanda alipelekwa hospitali chumba cha mahututi na mguu wake ukakatwa kufuatia ajali mbaya pale mbuyuni. Wakaazi wa Maganye wamezipata arafa hizi ispokuwa nyanyake na dadake, hatujui watazipokea vipi habari hizi za hali yake. watafanyaje? Hebu tupate fununu ya ilivyotokea katika kipindi hiki cha **"Kale walinikubali, sasa wananitenga".** Tunaanza hadithi yetu asubui mbichi jumaapili nyumbani kwa kina Karemi ambako Zabibu, msichana zeruzeru anamtazama nyanyake akifua nguo.

## SCENE ONE: SUNDAY MORNING AT KAREMI'S HOME

1. **SFX: WASHING OF CLOTHES BY HAND; BIRDS; YARD AMBIENCE**

2. **ZABIBU:** Nyanya Theresa, maisha ya Oluanda yatakuwaje sasa?

3. **THERESA:** Zabibu, sasa ni swali gani hilo? Hmm, nitajuaje maisha ya Oluanda? Mimi si mtabiri.

4. **ZABIBU:** Naelewa nyanya, lakini nilimaanisha.. je, kama…

5. **THERESA:** **(Cuts her short)** Kwani hujui wewe ? Sote twajua vile Oluanda ataishia baada ya kukatwa mguu wake…. Kwa ushahidi zaidi, nenda madukani ukashuhudie maskini wakiombaomba, hivyo ndivyo itakavyokuwa kwa Oluanda.

6. **ZABIBU:** Inasikitisha. Oluanda ni mmoja wa vijana wazuri hapa Maganye. Nyanya, kwanini wale walio na hali za ulemavu pekee ndio wameachwa wawe omba-omba Maganye?

7. **THERESA:** Zabibu,leo umenuia kunitia wazimu na maswali yako? Ntakujibu, Ni kwa sababu jamii kwa ujumla imewetenga na kusahau kuwa wao pia ni wanadamu wanaostahili kupewa haki na nafasi za kujimudu kimaisha. Na kwa vile ni lazima wajikimu basi husalia kuomba-omba.

**8. ZABIBU:** Lakini nyanya Theresa, watu hapa Maganye hunichukulia tofauti kwa sababu ya rangi ya ngozi yangu na macho. Hunikejeli na kunibeza kwa kila aina ya majina. **(more cheekily)** Lakini wakinichokoza, pia mimi nawachokoza.. kuna mvulana mwengine shuleni huwa yuwapenda kuniita 'mzungu', na yeye haoni masikio yake makubwa na marefu, mimi humwambia masikio yake yanasikia mvua ikitaka kunyesha siku moja kabla inyeshe…
**(They both laugh )**

**9. THERESA:** Mungu hakupi vyote,lakini wengi hawajui hivyo. Lakini Zabibu usimchokoze. Sikutarajia wewe uwe mchokozi, tabia hizo zinafanana na Karemi, sio wewe! Yuko wapi hivi sasa? Angelinisaidia kuanika hizi nguo kasha aende kumsaidia Oluanda kurudi nyumbani kutoka hospitali, kwani anatoka leo. **(calls out loudly)** Karemiiii!

**10. SFX:** **Steps coming closer**

**11. KAREMI:** **(approaching)** Naam, nyanya. Kelele hizo zote za nini, kwani mimi ni kiziwi? Waniita kwa tarumbeta mpaka watu wote Maganye wasikie nikiitwa?

**12. THERESA:** Usinisemeshe hivyo! Wajua nini kuhusu viziwi? Hebu nianikie hizi nguo, niharikishe kuenda

kanisani. Na ukumbuke kufika mapema hospitali kumsaidia Tofu amtoe Oluanda hospitali. **(sighs)** Sikilizeni wajukuu zangu. Sitaki mumtenge Oluanda hivi sasa, kwanza nataka muzidi kumuonyesha upendo na mumkubali, sasa ndio anawahitaji zaidi.

13. **KAREMI / ZABIBU:** Ndio nyanyaTheresa.

14. **MSIMULIZI:** Wahenga walisema: “wakionacho wakongwe wakiwa wameketi; vijana hawakioni wakiwa wamesimama” . haya ni swadakta kwa nyanya  Theresa, miongo mingi aliyoishi chini ya jua kali, ilimfunza kuwa mtu akizaliwa na ulemavu au apate ulemavu kupitia ajali kama vile Oluanda, magonjwa, vita, au kwa njia nyengine.. Wapungukiwa hawa hujikuta katika hali ngumu ya kimaisha. Lakini aliwanasihi wajukuu wake kuwaheshimu na kuwapa hadhi, na utu. Je utu-bora huu wake unatokana na nini? Ni kwa sababu ana mjukuu ambaye ni zeruzeru au kuna mengine? Endelea kusikiliza, kwa sasa tuangazie kule hospitali….

**<u>SCENE TWO: AT THE HOSPITAL ENTRANCE</u>**

15. **SFX: HOSPITAL AMBIENCE**

16. **SOUND OF WOODEN CRUTCHES USED FOR WALKING**

17. **OLUANDA:** **(Takes deep breath)** Efu!!

18. **TOFA:** Kwani hayo magongo ni mazito mwanangu? Sijui

kwanini wamekupa ya mbao. Nikipata pesa nitakununulia ya plastiki.

| | | |
|---|---|---|
| **19.** | **SFX:** | **WIDE DOOR OPENS - SWINGS FROM SIDE TO SIDE** |
| | | **(Karemi enters)** |
| **20.** | **KAREMI:** | **(Sudden outburst)** Ooooo ..Luanda..Unaendeleaje? shikamoo Mama Oluanda. Samahani Oluanda nimechelewa. |
| **21.** | **OLUANDA:** | Salama Karemi. Sina neno, najizoeza haya magongo. Dkt Esther amesema itanicukuwa muda mrefu kujuwa kuyatumia. |
| **22.** | **TOFA:** | Ndio,lakini kijana wangu ni jasiri, sindio? |
| **23.** | **OLUANDA:** | **(Trying to calm him down)** Mama tafadhali usinihurumie!.Sihitaji huruma ya mtu.. sawa? |
| **24.** | **KAREMI:** | **(Trying to calm him down)** Basi tulia... usisahau unazungumza na mamako. |
| **25.** | **TOFA:** | **(Starts to weep)** |
| **26.** | **OLUANDA:** | **(Still angry)** Ngazi! Pandio na pandio!..alaaniwe aliyeijenga hii hospitali na ngazi kila mahala. Watu kama mimi watatembea vipi na ngazi hizi? Wanadhani tuna mbawa kama ndege? |

27. **KAREMI:** Oluanda, acha basi nikusaidie..

28. **OLUANDA:** **(Cuts him short)** Sitaki msada wako! Ulikuja ili twende nyumbani ama? Basi twendeni!.

29. **MSIMULIZI:** Tofa na Karemi hawakuamini jinsi Oluanda alivyowageukia. Hakua yule mtulivu, mtiifu waliyemtambua kitambo. Amebadilishwa na nini? Wataweza kumuelewa kweli? Usikae mbali upate uhondo zaidi. Chitoto alikua ashasikia kuhusu kukatwa kwa mguu wa Oluanda na hisia za hukumu zikimjaa, akaamuwa kumueleza babake Fagilio.

30. **SFX: HEAVY SNORING**

31. **CHITOTO:** **(Excited)** Baba! Amka … hebu amka!

32. **FAGILIO:** **(Drunk voice)** Hmm.. Nini! Kwani polisi wametuvamia? Ficha pombe haraka!

33. **CHITOTO:** La, ni zaidi ya hilo! Sijui nikueleze nini baba.

34. **FAGILIO:** Nini? Kwani kuna nini mwanangu. Hmm.. nieleze...

35. **CHITOTO:** Lakini baba niahidi kuwa utaiweka siri..

36. **FAGILIO:** **(Excited)** Nishajuwa mpaka mwisho wako.. umeweka msichana wa watu mimba? Wataka kuitwa baba pia wewe? Ni msichana gani?

37. **CHITOTO:** Baba.. si..sii

**38. SFX : HEAVY SNORING**

**39. CHITOTO:** **…** Sivyo unavyofikiria….

**40. MSIMULIZI:** Kwa hviyo Chitoto alisalia kusimama pale akimtazama babake aliyekuwa kalewa chakari kama kawaida yake daima dawamu, ilikuwa nadra yeye kuwa macho makavu bila ya pombe. Atamuarifu nani sasa? kwengineko, Tofa ,Oluanda na Karemi walifika nyumbani, na pale rafiki yake Magoto alikua tayari yuwangoja ..

**<u>SCENE FOUR : OUTSIDE OLUANDA'S HOME</u>**

**41. SFX: OUTSIDE AMBIENCE; BIRDS; CHICKEN WOODEN CRUTCHES SLOWLY MOVING FOLLOWED BY WHISTLE USED BY THE FOUR FRIENDS.**

**42. MAGOTO :** **(Cowardly)** Naam Oluanda, ni.. ni.. vizuri kukuona... ehm unajisikiaje?

**43. OLUANDA:** **(Excited)** Ah nashukuru, ndugu yangu Magoto nimejifunza. Usilalamike safari ni ndefu. Wewe tembea. Uwe na miguu miwili, au mmoja. Maisha lazima yaendelee.

**44. TOFA:** Oluanda, huwakaribishi wageni wako ndani? Karemi, Magoto tafadhali karibuni ndani.

| | | |
|---|---|---|
| **45.** | **KAREMI:** | La, hapana, mama Oluanda, nimemuacha Zabibu pekee na nahitaji kurudi kabla nyanya hajarudi kutoka kanisani na kunikosa . Oluanda, vyema umerudi. Nitakuona wakati mwengine. |
| **46.** | **MAGOTO:** | Nafikiri pia mimi nitawaacha, ndio.. nitakuona wakati mwengine Oluanda. |
| **47.** | **OLUANDA:** | Hmm.. sawa. Nashukuru kwa kunitembelea... |
| **48.** | **SFX:** | **Footseps of two people leaving** |
| **49.** | **SFX:** | **DOOR UNLOCKED…THEN LOCKED** |
| **50.** | **TOFA:** | Magoto anaonekana kama anakuogopa.. hakuwa hali yake ya kawaida... |
| 51. | **OLUANDA:** | Simlaumu. Mimi mwenyewe najiogopa. Naogopa maisha ya mbeleni, nayaogopa haya magongo, naogopa kila kitu. Sina maana tena, ni heri ningelikufa! |
| **52.** | **TOFA:** | **(Shocked)** Oluanda! Unasubutu vipi… |
| **53.** | **SFX:** | **KNOCKING ON WOODEN DOOR** |
| **54.** | **TOFA:** | **(Sighing heavily)** Hmm Nani tena? Marafiki zako wote si washakutembelea? Hebu keti nitaufunguwa mimi mlango. |

**55. MSIMULIZI:** Swali zuri, je, huyo ni nani? Lakini amini usiamini, Kangwa msichana mrembo kuliko wote Maganye kasimama mbele ya kizingiti cha mlango wa Tofa, na alikua amekuja kumtazama Oluanda. Sikiliza kutatokea nini....

**56. SFX:** **MORE KNOCKING ON WOODEN DOOR**

**57. TOFA:** Wewe ni nani? Karemi,ni wewe?

**(SILENCE)**

**58. SFX:** **DOOR BEING UNLOCKED**

**59. KANGWA:** **(Shyly)** Shikamoo Mamake Oluanda, nilikuwa nimekuja kumuona Oluanda. Nilisikia ametoka hospitali…

**60. TOFA:** **(In a bit of shock)** Eeeh.. ndio.

61. **OLUANDA:** **(From inside)** Mama… ni nani?

**62. SFX:** **Steps going back to the room**

**63. TOFA:** **(Pleasantly, in a lower voice)** Ni Kangwa, Kangwa amekuja kukuona Oluanda.

**64. OLUANDA:** **(Gets hysterical, pressed voice)** Kangwa!..., Hapana mama! Atanionaje nikiwa hivi? Mama tafadhali mwambie aende! Mwambie siko!

**65. TOFU:** Oluanda, una nini lakini? Kangwa amekuja tu.. kuku....

**66. OLUANDA:** **(shouts )** Sitaki! Sitaki kuonekana, sitaki yeye wala mtu yeyote anione!

**67. SFX: Steps returning to the front door**

**68. TOFA:** **(Lovingly)** Kangwa, pole mwanangu, tangu hii ajali impate, Oluanda amegeuka kabisa. Tabia zake sizo kabisa. Mimi mwenyewe simuelewi..

**69. KANGWA:** **(Sadly)** Naelewa, mwambie namtakia kupona kwa haraka ili ajiunge nasi shuleni hivi karibuni..

**70. TOFA:** Asante sana, Nitamueleza .Wasalimie wazazi wako na samahani kwa yaliotokea.

**71. KANGWA:** Ni sawa. Ni vigumu kufikiria yanayomsibu kwa sasa..

**HITIMISHO:**

Ni bayana. Hakuna aliyejuwa yaliyokuwa yakipita akilini mwa Oluanda. Baada ya kupoteza mguu wake, alihisi uchungu, alihukumika, kupoteza tumaini, alijiona mnyonge na asiyependeza tena machoni mwa watu. Marafiki zake pia hawakusaidia. Na kwa hilo, tunahitimisha kipindi chetu cha leo. Je, yapi yatamtokea Oluanda? Kweli atarudi shule? Changamoto hili litaupa mwelekeo upi uhusiano wake na mamake? Kwa haya na zaidi usikose kipindi kifuatacho cha hadithi yetu ya redio kuhusu " **Ulemavu barani Afrika**". Unapotaka kusikiliza tena kipindi hiki au chengine kilichotangulia tembelea tovuti zetu www.dwworld.de/lbe**.** Mpaka hapo tena. Siku njema.